

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA SONGEA (“Songea WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-004

Mnamo tarehe 17 Mei 2018, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Songea (Songea WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina za wateja	Matumizi (M3)	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
		2017/18	%	2018/19	%	2019/20	%	2020/21
			Badiliko		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	0-10	895	17%	1,050	14%	1,200	4%	1,250
	10<-25	970	13%	1,100	14%	1,250	4%	1,300
	>25	1,000	15%	1,150	13%	1,300	1%	1,310
Biashara	0-10	1,000	15%	1,150	11%	1,280	2%	1,300
	>-10	1,075	12%	1,200	8%	1,300	6%	1,380
Taasisi	0-20	925	15%	1,060	19%	1,260	4%	1,310
	>20	1,000	15%	1,150	13%	1,300	4%	1,350
Viwandani	0-10	1,000	15%	1,150	11%	1,280	8%	1,380
	>10	1,075	16%	1,250	8%	1,350	4%	1,400
Kioski/Stand pipe		500	0%	500	0%	500	0%	500

Jedwali 2: Gharama ya Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (shilingi/mwezi)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
	2017/18	%	2018/19	%	2019/20	%	2020/21
		Badiliko		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	3,000	-100%	0	0%	0	0%	0
Biashara	4,000	-100%	0	0%	0	0%	0
Taasisi	3,500	-100%	0	0%	0	0%	0
Viwandani	4,500	-100%	0	0%	0	0%	0

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
	2017/18	%	2018/19	%	2019/20	%	2020/21
		Badiliko		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa
Biashara							
Taasisi							
Viwandani							

Jedwali 4: Bei za sasa na Zinazopendekezwa za Kuhamisha Maungio (TZS/Mwezi)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
	2017/18	%	2018/19	%	2019/20	%	2020/21
		Badiliko		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	15,000	20%	18,000	11%	20,000	10%	22,000
Biashara	15,000	20%	18,000	11%	20,000	10%	22,000
Taasisi	15,000	20%	18,000	11%	20,000	10%	22,000
Viwandani	15,000	20%	18,000	11%	20,000	10%	22,000

Jedwali 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Bei zilizopendekezwa					
	2017/18	%	2018/19	%	2019/20	%	2020/21
		Badiliko		Badiliko		Badiliko	
Majumbani	355	13%	400	0%	400	0%	400
Biashara	625	4%	650	4%	675	4%	700
Taasisi	600	4%	625	4%	650	4%	675
Viwandani	630	3%	650	4%	675	4%	700

Table 6: Tozo za sasa na zinazopendekezwa kwa ajili ya huduma ya gari la maji taka (CESSPIT EMPTIER)

Aina za Wateja	Umbali	Bei za sasa	Tozo zinazopendekezwa					
		2017/18	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20	% Badiliko	2020/21
Wateja wote	0-10	60,000	8%	65,000	15%	75,000	0%	75,000
	10<-20	70,000	7%	75,000	13%	85,000	0%	85,000
	20<-30	80,000	6%	85,000	12%	95,000	0%	95,000

Kutokana na wasilisho la Songea WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kuongeza mapato ili kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, kupanua mtandao wa usambazaji majisafi kwenye makazi mapya na kuweza kupata fedha za kulipia uchakavu wa miundombinu ya majisafi.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 5 Julai, 2018, katika Ukumbi wa Manispaa, Songea Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya **tarehe 19 Julai, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au ofisi za Songea WSSA zilizoko mjini Songea.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
11 Juni 2018